

BODI YA USAJILI WA WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI MAJENZI

(Architects and Quantity Surveyors Registration Board)

(Under Act No.4 of 2010)



TAARIFA KWA UMMA

Kuhusu Uuzaji Holela Wa Ramani Za Majengo

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) inatoa onyo kali kwa watu Wanaochora na Kuuza Ramani/Michoro ya Ubunifu Majengo na Kusambaza katika Vitabu, Majarida katika maeneo ya Barabara, Mitandao Ya Jamii kama Facebook, Instagram N.K.

Aidha, Bodi inatoa **Tahadhari** kwa wananchi wote kutonunua au kutumia Michoro hiyo ambayo imebuniwa na watu wasiosajiliwa na kutambulika kisheria na hivyo Viwango vya Usalama wake kutofahamika. Hivyo kutumia michoro hiyo si tu kinyume na sheria bali pia kunaweza kuleta madhara katika matumizi yake.

Ikumbukwe kuwa michoro yoyote ya ujenzi hufanywa na wataalam wenye sifa na kusajiliwa kisheria ili kuhakikisha zinafuata maadili ya kazi na kukidhi viwango vya ujenzi wa jengo husika, kwa kuzingatia matumizi mbalimbali ya watumiaji na eneo husika.

Ifahamike kuwa si kila ramani ya jengo inafaa katika kila eneo la ujenzi kwani kila eneo la ujenzi lina mazingira tofauti kama ikiwa ni pamoja na hali ya hewa, miundo mbinu iliyopo, miteremko, aina ya udongo, matumizi ya jengo n.k. Kwa maana hiyo tunasisitiza katika uchoraji wa jengo wananchi washirikishe Wataalam waliosajiliwa watakaoweza kubuni michoro inayoendana na mazingira ya eneo husika.

Aidha, Bodi inawataka watu wote wanaojihusisha na **Kuchora na Kuuza Ramani Za Majengo Kinyume Na Sheria Kuacha Mara Moja**, na endapo watakaidi onyo hili, **Bodi** itawachukulia

hatua kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriji Majenzi Na.4/
2010.

IMETOLEWA NA KAIMU MSAJILI

BODI YA USAJILI WA

WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI MAJENZI (AQRB)

S. L. P. 72673 Dar es Salaam.

Simu: 255 (022) 2110292, 2117546, Nukushi: 255 (022) 2117535

Barua pepe: info@aqrb.go.tz, Tovuti: www.aqrb.go.tz